
Sheria ya kufunga Watoto mikanda ya Jimbo la New York - *Mikanda ya kufunga abiria watoto ni Lazima, Ni Sheria!*

Watoto wote lazima wafungwe katika mikanda sahihi ya kuzuia mtoto wakati wakiwa kwenye gari, **hadi kufikia miaka nane.**

Kifaa sahihi cha kuzuia watoto ni ambacho kina saizi na uzito wa mtoto uliopendekezwa na mtengenezaji.




**Umri unaofaa unatofautiana kwa kila aina ya kiti ili kuweza kuendana na utofauti katika ukuaji wa mtoto na ukomo wa kimo/uzito wa viti na viti vya nyongeza.Tumia mwongozo wa mmiliki wa kiti cha abiria au mwongozo wa mmiliki wa kiti cha nyongeza ili kuzingatia ufungaji na urefu wa kiti /uzito, na matumizi sahihi ya kiti.* Ikiwa mtoto ana umri wa miaka nane na ni chini ya 4'9 " kwa urefu au ana uzito wa chini ya pauni 100, inapendekezwa kuendelea kutumia mfumo wa kuzuia watoto.

## INAYOANGALIA NYUMA

Kiti cha abiria cha Mtoto

**Kuzaliwa mpaka miaka 2***

Mtoto husafiri akiangalia nyuma kwenye kiti cha nyuma kama amefungwa hadi miaka 2 au mpaka kufikia uzito wa juu au kimo cha urefu wa kiti hicho cha abiria. (viti vinavyoweza kubadilishwa vinaweza kutumiwa vikiangalia nyuma au mbele)

**Inayoangalia mbele kwa sehemu ya kufunga**

Funga mikanda kwa mabega au chini ya mabega

Funga sehemu ya kati katika sehemu ya kifua kati ya makwapa

Funga sehemu ya chini kupitia kwenye nyonga na sio tumboni

**Uwekaji***

Kiti cha abiria mtoto kinachoangalia nyuma lazima kushikamana na kiti cha gari na mkanda wa kiti cha gari au nanga za chini. Viti vya abiria watoto vilivyowekwa vizuri havipaswi kusonga zaidi ya inchi moja upande kwa upande na mbele kuelekea nyuma.

Kamwe usiweke kiti cha abiria mtoto mbele ya mfuko ya hewa.

## INAYO ANGALIA MBELE

Kiti cha abiria cha Mtoto

**Umri wa miaka 2 mpaka miaka 5***

Wakati mtoto anakuwa na kupita kiti kinachoangalia nyuma wanapaswa kusafiri kwa kutumia kiti kinachoangalia mbele na kutumia mshipi hadi angalau umri wa miaka 5 au mpaka kufikia uzito wa juu au kikomo cha urefu wa kiti cha abiria cha mtoto. (viti vinavyoweza kubadilishwa vinaweza kutumiwa vikiangalia nyuma na kuangalia mbele/ Viti vilinyounganishwa ni mchanganyiko wa viti vinanyoangalia mbele inayojifunga na ya kuongeza)

**Inayoangalia mbele kwa sehemu ya kufunga**

Funga mikanda kwa mabega au juu ya mabega

Funga sehemu ya kati katika sehemu ya kifua kati ya makwapa

**Uwekaji***

Kiti cha abiria mtoto kinachoangalia mbele lazima kushikamana na kiti cha gari na mkanda wa kiti cha gari au nanga za chini. Viti vya abiria watoto vilivyowekwa vizuri havipaswi kusonga zaidi ya inchi moja upande kwa upande na mbele kuelekea nyuma.

Kamwe usiweke kiti cha abiria mtoto mbele ya mfuko ya hewa.

## KITI CHA NYONGEZWA

**Miaka 4-7***

Inapendekezwa mtoto kusafiri akitumia kiti cha nyuma cha watoto kinacho angalia mbele pamoja na kufungwa hadi kufikia urefu wa juu au kikomo cha uzito kinachoruhusiwa na mtengenezaji wa kiti.

Wakati mtoto amekuwa kupita kiti cha gari cha watoto kinachofungwa, kiweke kwenye kiti cha nyongeza, akiwa kwenye kiti cha nyuma cha gari. Viti vilivyounganishwa ni mchanganyiko wa kitu cha kukalia ukiangalia mbele kama umefungwa na ya kuongezea

**Nafasi ya ukanda wa kiti cha nyongeza:**

1. UMkanda wa bega ulala kwenye bega na kifua na sio shingoni au uso.
2. Mkanda wa bandari hupitia kwenye mapaja ya juu (sio tumbo).

**Uwekaji***

Viti vya nyongeza hutumia mkanda wa kiti ili kuzuia mtoto na kusaidia kuongoza mkanda mbali na shingo na uso wa mtoto na kumwinua mtoto kwa nafasi ambayo inaweka mkanda wa tumbo mbali na tumbo.

Ikiwa kuna mkanda kwa kiti cha nyongeza shikanisha na gari.

## MKANDA WA KITI

**8 - miaka 12 na zaidi***

Mkanda wa usalama katika gari lako haujaundwa kwa watoto. Mazoea bora yanaonesha kwamba watoto ni salama ikiwa hutumia kiti cha nyongeza mpaka ukanda wa kiti unatoshea vizuri.

**Kanda za viti hutoshea vizuri wakati:**

1. Mkanda wa bega umelala kwenye bega na kifua na sio kupitia shingo au uso.

2. Mkanda wa bandari hupitia kwenye mapaja ya juu (sio tumbo).

3. Watoto wanapaswa kuwa warefu ili kwa urahisi kupiga magoti kupita kando ya kiti ya nyuma na mgongo dhidi ya kiti cha gari.

Inapendekezwa sana kwamba watoto wote wenye umri wa miaka 12 na chini kusafari wakiwa wamefungwa vizuri katika kiti cha nyuma.

Kiti cha mbele, dereva na kila abiria lazima kuvaa mkanda wa kiti, mtu mmoja kwa kila mkanda. Dereva na abiria wa mbele wenye umri wa miaka 16 au zaidi wanaweza kutozwa faini ya hadi $ 50 kila mmoja kwa kuto kuvaa mkanda wa kiti.

**Kila mmiliki, bila kujali umri au sehemu wanapokaa lazima kufungwa na kuzuizi cha usalama. Kila abiria chini ya umri wa miaka 16 anatakiwa kuvaa ukanda wa kiti au kutumia mfumo sahihi wa kuzuia mtoto. Dereva lazima ahakikishe kwamba kila abiria chini ya umri wa miaka 16 anatii sheria. Dereva anaweza kufainiwa $ 25 hadi $ 100 na kupokea alama za adhabu za leseni za dereva kwa kila ukiukwaji.**

**TS.CPS.2017.Swahili.CPS Seat Chart Flyer 11 x 17**

Child passenger seat recommendations: American Academy of Pediatrics Safety Committee. Graphic design: adapted from National Highway Traffic Safety Administration. This flyer was modified Aug 2017 by Mohawk Valley Resource Center for Refugees with recommendations from the New York State Governors Traffic Committee. Translations provided by **Tone** at www.tonetranslate.com a division of Mohawk Valley Resource Center for Refugees. This project is made possible through theMohawk Valley Resource Center for Refugees' Child Passenger Safety program funded by the National Highway Traffic Safety Administration with a grant from the New York State Governor's Traffic Safety Committee.

NEW YORK STATE OF OPPORTUNITY. Governor's Traffic Safety Committee

MVRCR MOHAWK VALLEY RESOURCE CENTER FOR REFUGEES

tone